

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

(VETA)



MKATABA WA KUTENGENEZA NA KUFITISHA MILANGO (DOOR SHUTTER) UJENZI WA  
CHUO CHA VETA MKINGA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 11 mwezi 03 .....mwaka 2022

KATI YA

Mkurugenzi wa Kanda, VETA Kanda ya Kaskazini, S.L.P. 1738, Moshi, ambaye anaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802, Dodoma (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

ABDUL FUNYO CO. LTD, wa S.L.P 1793, TANGA (ambaye katika Mkataba huu ataitwa "MZABUNI" kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri anajenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni kwa ajili ya kazi ya kuweka na kufitisha milango (Door shutter) katika ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Mzabuni mchanganuo wa kazi za kutengeneza na kufitisha milango pamoja na nakala ya michoro katika Ujenzi wa Chuo cha VETA Mkinga.

NA KWA KUWA Mzabuni amekubali kwa hiari yake kufanya kazi ya kutengeneza na kufitisha milango (door shutter) katika Ujenzi wa Chuo cha VETA Mkinga.

Hivyo basi pande zote mbili zinakubaliana na masharti yaliyopo hapa chini kama ifuatavyo:-

**PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KWAMBA:-**

1. Maelezo ya kazi:-
  - 1.1. Gharama ya kutengeneza na kufitisha milango (door shutter) Tzs. 58,340,000.00 (kwa maneno Milioni Hamsini na nane laki tatu na arobaini elfu na senti sifuri tu fedha za Kitanzania) kwa majengo kumi na mbili (12) ambayo ni jengo la Utawala (1), Jiko na bwalo (1), Nyumba ya Mkuu wa Chuo (1), Nyumba ya familia mbili (1), Kibanda cha Mlinzi (1), Vyoo vitatu (3), Stoo (1), nyumba ya umeme (1) na mabweni mawili (2).
  - 1.2. Kwamba, Mkataba huu utakuwa wa mwezi mmoja, kuanzia tarehe atakayokabidhiwa kazi.
  - 1.3. Kazi itafanyika kutokana na oda (LPO) utakayopewa.
  - 1.4. Mzabuni anatakiwa azingatie vipimo kwa usahihi kulingana na maelekezo ya kazi.
  - 1.5. Kama kuna mabadiliko katika Mkataba (variations), mabadiliko haya yatawasilishwa kwa njia ya maandishi na pande zote mbili zinazohusika zitakubaliana namna ya utekelezaji wa mabadiliko hayo.
2. Kipindi cha utekelezaji:
  - 2.1. Kwamba, wakati wa utekelezaji wa mkataba huu mwajiri anaweza kuongeza muda wa mkataba iwapo kutakuwa na sababu zitakazodhihirika kuwa ni sababu za msingi na zisizozuilika.
3. Malipo kwa Mzabuni
  - 3.1 Mwajiri atalazimika kumlipa Mzabuni malipo yote ya kazi aliyofanya baada ya kupata hati ya uthibitisho wa kufanya malipo kutoka kwa Mhandisi msimamizi wa mradi.
  - 3.2 kwamba, Mzabuni atakiri kwa maandishi kulipwa malipo hayo ndani ya siku tatu (3) baada ya kupokea malipo.
4. Msimamizi wa Mkataba huu atakuwa Mhandisi wa mradi (Site Engineer).
5. Ubora wa kazi:

Mzabuni atatekeleza kazi kwa ubora, uaminifu na kulingana na viwango vya ubora unaokubaliwa na Mwajiri. Kazi ambayo itakuwa haina ubora na kiwango kinachohitajika na Mwajiri, itarekebishwa na Mzabuni kwa gharama zake.
6. Usalama wa wafanyakazi:

Mzabuni anatakiwa kuhakikisha usalama wa wafanyakazi wake mwenyewe. Mwajiri hatahusika na madai yoyote ya fidia yatakayotokea katika eneo la kazi.

7. Kuvunja Mkataba:

- 7.1. Mwajiri ana haki ya kuvunja/ kukatisha Mkataba bila ya malipo iwapo Mzabuni atafanya kazi isiyoridhisha, kazi iliyochini ya kiwango au Mzabuni kushindwa kutekeleza makubaliano ya Mkataba.
- 7.2. Kama kutatokea kutoelewana/mgogoro kati ya mwajiri na Mzabuni, usuluhishi (Arbitration) wa pande hizi mbili utafanywa kwa mazungumzo ya pamoja ya kutafuta muafaka na kama muafaka utakosekana kwa njia ya mazungumzo basi mmoja kati yao anaweza kupendekeza kuamua mgogoro utatuliwe kwa njia rasmi ambazo ni usuluhishi kwa kutumia mtu wa tatu ambaye pande zote mbili zitaridhia.

8. Sheria zitazotumika:

Mkataba huu, tafsiri yake na mahusiano baina ya Mwajiri na Mzabuni yatatekelezwa kwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


IMESAINIWA NA KUWEKWA MUHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA MKURUGENZI WA KANDA, VETA KANDA YA  
KASKAZINI

Jina: MONICA MBELLE

Saini: 

Wadhifa: MKURUGENZI WA KANDA

Tarehe: 11/03/2022




Mbele ya (Shahidi)

Jina: Odelairumbe Ci

Saini: 

Wadhifa: Principal

Tarehe: 11/03/2022



IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: ABDUL S. MWANAFUNTO

Saini: 

Wadhifa: DIRECTOR

Tarehe: 11/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: OMARI SELEMAN KIMWERI

Saini: 

Wadhifa: SHAHIDI WA MZABUNI

Tarehe: 11/03/2022